

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**



**MKUTANO WA TATU**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA NNE**

**22 APRILI, 2016**

**MKUTANO WA TATU - YATOKANAYO NA KIKAO CHA NNE**  
**TAREHE 22 APRILI, 2016**

**I. DUA**

Saa 3.00 asubuhi Mhe. Dkt. Tulia Ackson (NAIBU SPIKA) alisoma Dua na kuliongoza Bunge

**Makatibu Mezani**

1. Ndg. Ramadhani Abdallah
2. Ndg. Lawrence Makigi
3. Ndg. Asia Minja

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani:-

- Mhe. Jenista Joakim Mhagama aliwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa aliwasilisha Taarifa ya Kamati hiyo kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI Mhe. Sikuzani Yassin Chikambo aliwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya Uratibu na Udhhibiti wa Dawa za kulevya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI) kwa Mwaka 2016/2017.

**III. MASWALI**

Maswali yafuatayo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge:-

**1. OFISI YA WAZIRI MKUU**

Swali Na.31: Mhe. Khalifa Mohammed Issa

Swali la nyongeza: Mhe. Khalifa Mohammed Issa

**2. OFISI YA RAIS (TAMISEMI)**

Swali Na. 32: Mhe. Salma Mohammed Mwassa

Swali la nyongeza: Mhe. Salma Mohammed Mwasa

Swali Na. 33: Mhe. Aida Joseph Khenani

Swali la nyongeza: Mhe. Aida Joseph Khenani

Mhe. Dkt. Raphael Chegeni

**3. WIZARA YA NISHATI NA MADINI**

Swali Na. 34: Mhe. Oran Manase Njenza

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Oran Manase Njenza  
(ii) Mhe. Joseph Leonard Haule  
(iii) Mhe. Juma Selemani Nkamia

**4. WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI**

Swali Na. 35: Mhe. Boniface Mwita Getere

Swali la nyongeza: Mhe. Boniface Mwita Getere

**5. WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Swali Na. 36: Mhe. Neema William Mgaya

Swali la nyongeza: Mhe. Neema William Mgaya

**6. WIZARA YA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA:**

Swali Na. 37 Mhe. Hafidhi Ali Tahir

Swali la nyongeza: Mhe. Hafidh Ali Tahir

**7. WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Swali Na. 38: Tunza Issa Malapo

Swali la nyongeza: Mhe. Tunza Issa Malapo

Swali Na. 39: Mhe. Rashid Mohamed Chuachua (kny. Mhe. Jerome Dismass Bwanausi)

Swali la nyongeza: Mhe. Rashid Mohamed Chuachua.

Swali Na. 40: Mhe. Josephine Johnson Genzabuke

Swali la nyongeza: Mhe. Josephine Johnson Genzabuke.

**MATANGAZO:**

**WAGENI:**

1. Wageni walioko kwenye Gallery walitambulishwa Bungeni;
2. Wabunge ambao hawajachukua Passport zao wakachukue Idara ya Itifaki;
3. Swali Na. 33 la TAMISEMI lilichanganywa majibu yakatolewa ya Arumeru badala ya Rukwa Hivyo swali hilo litapewa nafasi ya kujibiwa wakati mwingine.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

Waziri Mkuu alitoa Hoja kwamba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/17. Hoja hiyo iliungwa mkono.

#### **MATANGAZO:**

Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni alitangaza kwamba Kamati ya Utendaji ya CPA ikutane saa 8.00 katika ukumbi wa Spika.

Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria) alisoma maoni ya Kamati hiyo kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mhe. Consntine John Kanyasu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI aliwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Tume ya Uratibu na Udhhibiti wa Dawa za Kulevya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

#### **V. KUSITISHA BUNGE:**

Saa 6.59 mchana Mhe. Spika alisitisha kikao cha Bunge hadi saa 11.00 jioni.

**VI.** Bunge lilirudia saa 10.00 jioni na Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe aliwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mwenyekiti alieleza kuwa Taarifa ya Upinzani haijajielekeza kwenye Hoja ya Msingi ya Hotuba ya Waziri Mkuu na kama kuna Sheria imevunjwa kama ilivyoelezwa na Msemaji taratibu za Kisheria zifuatwe na mjadala uliopo mbele ya Bunge uendelee kwani mwenye Mamlaka ya kutafsiri Sheria au kama Katiba imevunjwa ni Mahakama.

#### **MJADALA WA JUMLA:**

Waheshimiwa Wabunge wafuatao walichangia

1. Mhe. Dkt. Diodorus Buberwa Kamala - CCM
2. Mhe. Joseph Kizito Mhagama - CCM
3. Mhe. Omary Ahmed Badwel - CCM
4. Mhe. Raphael Japhary Michael - CHADEMA

**TAARIFA:**

Mhe. Ester Nicholas Matiko alitoa Taarifa kwamba Mbunge anayechangia anazungumza masuala ya Nishati na Maji wakati masuala hayo hayako chini ya Ofisi ya Waiziri Mkuu. Mhe. Omary Ahmed Badwel alikataa Taarifa hiyo na aliendelea kuchangia.

Mwenyekiti alimshauri mzungumzaji kuzingatia Hoja na si vinginevyo. Mhe. Raphael Japhery Michael aliendelea na kusisitiza kutoendelea kuchangia kama alivyosema Kiongozi wa Upinzani kwamba Kambi haiko tayari kushiriki uvunjaji wa Katiba, Sheria na Haki za Wananchi.

6. Mhe. Shabani Omari Shekilindi - CCM
7. Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa - CCM
8. Mhe. Ignas Aloyce Malocha - CCM
9. Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka - CHADEMA

Naye alisema hatachangia mpaka watakapopata maelekezo mengine kama alivyosema Kiongozi wa Upinzani.

10. Mhe. Ally Keissy Mohammed - CCM

**KUHUSU UTARATIBU:**

Mhe. Livingstone Joseph Lusinde aliomba mzungumzaji kulindwa wakati akichangia kwani Wabunge wengine ambao wamegoma kuchangia hawampi nafasi kwa kumingilia wakati anachangia.

11. Mhe. Desderius John Mipata - CCM
12. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda - CCM
13. Mhe. Mgumba Tebweta Omary - CCM
14. Mhe. Leonidas Tutubert Gama - CCM
15. Mhe. Juma Selemani Nkamia - CCM
16. Mhe. Leah Jeremiah Komanya - CCM
17. Mhe. Amina Saleh Mollel - CCM
18. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku - CCM

**TAARIFA**

Mhe. Masoud Abdallah Salim alitumia K.64 (f) (g) akisisitiza Mbunge kutumia Lugha ya Bunge na Mwenyekiti alieleza Kanuni aliyotumia siyo sahihi na kusisitiza Wabunge kuzingatia Kanuni ili Majadiliano yaende vizuri.

19. Mhe. Augustine Vuma Holle - CCM

## **KUHUSU UTARATIBU**

Mhe. Marwa Ryoba Chacha alitumia Kanuni ya 68(1) na 64(1)(b) kwamba Mbunge anachangia jambo ambalo haliko kwenye mjadala.

Mwenyekiti alisema mjadala ni mpana unagusa uchumi na siasa.

Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara alitumia Kanuni ya 68(1) na 64(1)(a) kwamba Mbunge anaechangia ameongea habari ambazo hazina ukweli kwani Wabunge wa Upinzani kutochangia hawajalazimishwa kufanya hivyo na alichowasilisha Msemaji wa Upinzani ni maamuzi ya Kikao cha Upinzani na siyo yake binafsi.

- |                                |       |
|--------------------------------|-------|
| 20. Mhe. Flatei Gregory Massay | - CCM |
| 21. Mhe. Jitu Vrajlal Soni     | - CCM |
| 22. Mhe. Issa Ali Mangungu     | - CCM |

## **VII. KUAHIRISHA BUNGE**

Saa 2.00 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Jumatatu tarehe 25 Aprili, 2016 saa 3.00 Asubuhi.

**DODOMA**  
**22 APRILI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH**  
**KATIBU WA BUNGE**